


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA  
SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA  
NJOMBE**



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na: NDC/PMU/3/VOL. III/07

Tarehe: 16/06/2023

**TANGAZO**

**MWALIKO WA ZABUNI**

**ZABUNI NA. LGA/031/2022/2023/D/01**

**UUZAJI WA MITI YA MIKARATUSI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anatoa mwaliko kwa Wafanyabiashara wa mazao ya misitu wenye uwezo wa kununua miti aina ya mikaratusi ishirini (20) yenye ukubwa wa vipimo vifuatavyo:-

S/NA	KIPENYO- DBH (SM)	UREFU (M)	UJAZO WA MITI (M <sup>3</sup> )	KIPIMO	IDADI
1	60	32	3.62	PC	1
2	58	26	2.75	PC	1
3	33	23	0.79	PC	1
4	38.5	15	0.70	PC	1
5	50	30	2.36	PC	1
6	63	33	4.11	PC	1
7	53	26	2.29	PC	1
8	45.5	24	1.56	PC	1
9	27	23	0.53	PC	1
10	48	35	2.53	PC	1
11	43	31	1.80	PC	1
12	35	23	0.88	PC	1
13	26	30	0.64	PC	1

14	28	24	0.59	PC	1
15	26	24	0.51	PC	1
16	23	25	0.42	PC	1
17	43	31	1.80	PC	1
18	38	23	1.04	PC	1
19	34	23	0.83	PC	1
20	35	22	0.85	PC	1
<b>JUMLA</b>			<b>30.6</b>		<b>20</b>

Miti hiyo ipo nyuma ya nyumba za Wakuu wa Idara ofisi za zamani za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Muombaji anakaribishwa kutembelea maeneo ilipo miti hiyo kwa gharama zake. Zabuni inatangazwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

**MASHARTI YA MWOMBAJI:**

1. Muombaji awe Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea au kampuni ya kitanzania
2. Mwombaji awe tayari kufanya tathmini ya kimazingira(EIA) kabla ya kuanza kazi ya uvunaji wa miti miti hiyo.
3. Mwombaji awe na vitendea kazi vya kutosha kumudu vyema kazi ya uvunaji miti pasipo kuhatarisha mali nyingine zilizipo jirani na miti hiyo.
4. Mwombaji atatakiwa kujaza na kuwalisha mchanganuo wa gharama ya ununuzi wa miti (mikaratusi) kulingana na mahitaji ya kotesheni.
5. Maombi yawe na maelezo na viambatanisho muhimu, yafungwe kwenye bahasha na kuandikwa 'Zabuni ya ununuzi wa miti' na itumwe kwa anuani ifuatayo:-

**KATIBU BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**

**S.L.P 547**

**NJOMBE**

6. Wafanyabiashara wenye uwezo na nia ya kununua miti wanakaribishwa kufika katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Njombe iliyopo Njombe Mjini karibu na Tanesco barabara ya Songea ili kuchukua kotesheni ya mchanganuo wa miti

Mwombaji atalipia kiasi cha Tsh. 20,000/= (elfu ishirini tu) wakati wa kuchukua kotesheni ambayo haitarudishwa.

7. Kwa wale wote watakao leta maombi yao kwa mkono barua zipelekwe ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU), iliyopo Njombe Mjini Ofisi za Halmashauri ya zamani (barabara ya Njombe - Songea karibu na Tanesco).
8. Mwisho wa kupokea maombi ni Ijumaa 23/06/2023 saa 4:30 na kufuatiwa na ufunguzi wa zabuni utakaofanyika saa 5:00 katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe karibu na Tanesco. Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni kwa gharama zenu.

  
Augustino Nyenza  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**NJOMBE**